

## **Kupunguzwa kwa malipo ya chekechea-barnehage / utunzaji wa mchana shuleni -SFO kuanzia Januari 2021**

### **CHEKECHEA**

**Kupunguzwa kwa malipo ya wazazi kwa familia au nyumba ambazo zinapokea mshahara chini ya krona 592.167 kwa mwaka**

Wale ambao wanaishi katika nyumba moja na mapato au mshahara wao kwa jumla/mwaka ni chini ya krona 592.167 kwa mwaka wanaweza kuomba ili walipe kidogo/wawapunguziye malipo ya chekechea. Kumbuka kwamba ikiwa una watoto kadhaa/wengi, ni lazima utume ombi kwa kila mmoja/mtoto kwa watoto hawa.

**Wakati wa msingi bila malipo kwa nyumba ambazo zina mshahara au mapato chini ya NOK 566.100 kwa mwaka**

Wakati wa msingi wa bure au bila malipo inamaanisha kwamba mtoto anapewa/hupata masaa 20 ya kushiriki/ kwenda katika chekechea kwa wiki bila malipo. Unaweza kupata mahali/fasi ya msingi bila malipo kutoka mwezi wa nane/Agosti ya mwaka ule mtoto wako anafikisha umri wa miaka 2 (myaka mbili ). Ikiwa au kama utaomba malipo ya mzazi yaliyopunguzwa, utapokea moja kwa moja nafasi/mahali ya msingi wa bure ikiwa msharaha/malipo ya konyumbani kwako iko chini/ndogo ya krona 566.000 kwa mwaka.

### **Utunzaji wa mchana - SFO**

**Kupunguzwa kwa malipo ya wazazi kwa nyumba zilizo kuwa na mshahara/mapato chini ya krona 505 083 kwa mwaka**

Wale ambao wanaishi katika nyumba au familia moja na mapato/msharaha yao kwa jumla/mwaka ni chini ya NOK 505 083 kwa mwaka wanaweza kuomba kupunguziwa malipo ya wazazi katika SFO.

**SFO bila malipo kwa watoto wa darasa la 1 kwa nyumba ambazo zina mapato au mshahara chini ya krona 350.000 kwa mwaka.**

Ikiwa unaomba kupunguziwa kwa malipo ya mzazi katika SFO, utapata SFO ya bure moja kwa moja ikiwa/kama mtoto wako yupo katika darasa la kwanza na nyumba yako ina mapato/mshahara amboyo iko chini ya krona 350.000 kwa mwaka.

### **Jinsi ya kuomba:**

Unaomba kielektroniki. Ambatanisha na nyaraka au karatasi halali/valide. Unaingia kwa kutumia kitambulisho rasmi - ID porten (Kitambulisho cha Benki-Bank ID, Kitambulisho Changu-MIN ID n.k.) kwa kutuma maombi yako.

**Fomu ya maombi ya chekechea inaweza kupatikana hapa:**

[www.bergen.kommune.no/redusert-foreldrebetaling](http://www.bergen.kommune.no/redusert-foreldrebetaling)

**Fomu ya maombi ya SFO inaweza kupatikana hapa:**

[www.bergen.kommune.no/redusert-foreldrebetaling](http://www.bergen.kommune.no/redusert-foreldrebetaling)

### **Je! Una watoto katika chekechea na pia utunzaji wa baada ya shule?**

Kama/Ikiwa una watoto katika chekechea na pia utunzaji wa baada ya shule, chagua fomu ya Maombi- Kupunguziwa chekechea na shule - *Søknadsskjema- Redusert foreldrebetaling barnehage og skole*. Hii utaipata chini ya alama fomu ya maombi unapobonyeza kwenye moja ya tovuti/viungo zilizo hapa juu.

### **Ni nyaraka zipi ambazo ni halali/valide:**

- Muhtasari wa malipo ya kodi (repoti ya malipo) - skattemelding - ya mwaka wa 2020 ya watu wazima katika nyumba ambayo mtoto anashi pamoja nao ni lazima iambatanishwe na barua ya maombi.
- Ikiwa/kama kuna mabadiliko makubwa katika mapato/mshahara yako kulingana na muhtasari/repoti ya malipo, unaweza pia kuambatanisha hati za malipo au mshahara kwa myezi 3 iliyopita.
- Ikiwa/kama umefutwa au umepoteza kazi, unaweza kuambatanisha nyaraka kutoka kwa mwajiri/boss.
- Uamuzi kuhusu msaada kutoka hazina(ofisi) ya mkopo wa kielimu -studie lånekassen na cheti cha mwanafunzi
- Uamuzi kutoka kwa NAV ya kijamii - sosial / kumalizika kwa uamuzi kutoka kwa NAV ya kijamii
- Ikiwa unasubiri ufafanuzi/mwangaza-avklaring kutoka kwa NAV, lazima ufahamishwe hii
- Habari zingine muhimu kuhusu mapato yako ya sasa

### **Sina muhtasari/repoti ya malipo ya kodi - skattemelding:**

Kila mtu ambaye amekuwa akiishi Norway kwa mwaka uliopita ana hati ya kodi au ripoti ya malipo /ushuru ni lazima aiambatishane na maombi hayo. Ikiwa/kama umefika tu Norway na hauna malipo ya ushuru, lazima uambatanishe kitambulisho (nyaraka za kibali) cha kuishi nchini Norway.

### **Maombi haya yanahusu kipindi gani:**

Maombi ya kupunguziwa kwa malipo ya wazazi yanahusu mwezi unaofuata baada ya maombi kupokelewa. Utatumiwa uamuzi( jibu) baada ya ombi lako kuidhinishwa/ kukubaliwa. Ikiwa/kama mtoto anahudhuria/ anaenda katika chekechea ya kibinafsi (prive), chekechea hio itapokea barua/nakala ya uamuzi huo.

### **Sina nambari ya usalama wa kijamii-personnummer / siwezi kuomba kielektroniki:**

Unaweza kuwasiliana au kuingeya na manispaa ya Bergen, Huduma ya Raia- innbyggjerservice katika Kaigaten 4, ili upate msaada wa kutuma maombi kielektroniki au kwa njia ya kawadia ikiwa/kama hauna nambari ya usalama wa kijamii. Leta kitambulisho halali na nyaraka zinazohitajika kwenye maombi. Huduma /ofisi ya raia ina nambari ya simu 55 56 55 55.

### **Muhimu! Kumbuka kuomba kila mwaka/ kumbuka kutuma barua ya ombi kila mwaka!**

Ni lazima utume ombi mpya ya kupunguziwa kwa malipo ya wazazi kila mwaka. Tuma maombi yako mapema! Omba mwezi wa Juni (sita) ili upate malipo yaliyopunguzwa katika mwezi wa agosti (nane).